

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**  
**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**  
(Ofisi: Jengo la Ushirika Mtaa wa Lumumba)

**Simu:** +255-22-2181344, 2180113, 2180141  
2180048,

**Nukushi:**+255-22-2180371

**Barua Pepe:** [usajili@brela.co.tz](mailto:usajili@brela.co.tz)  
[ceo@brela.go.tz](mailto:ceo@brela.go.tz)  
[brela@brela.go.tz](mailto:brela@brela.go.tz)



**S.L.P. 9393**  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUFUTWA KWA MAKAMPUNI (LIMITED BY GUARANTEE) YENYE KUFANYA SHUGHULI ZILIZOAINISHWA KWENYE SHERIA YA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGO'S)**

1. Kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Makampuni (SURA.212 ) yaliyofanyika kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ( Na. 3) ya mwaka 2019 iliyoanza kutekelezwa **tarehe 30 Juni 2019**, Jukumu la kusajili Makampuni yanayofanya shughuli kwa lengo la kutogawana faida na ambazo hazina malengo ya kukuza biashara" promotion of commerce" limehamishiwa kutoka kwa **MSAJILI WA MAKAMPUNI (BRELA)** kwenda Kwa Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's).
2. Kufuatia mabadiliko haya, **MSAJILI WA MAKAMPUNI (BRELA)** anapenda kuufahamisha umma na wamiliki wote wenye Makampuni ambayo yanafanya shughuli kwa lengo la kutogawana faida na ambayo **hayana** malengo ya kukuza biashara" Promotion of commerce" kwamba kampuni hizo zote zitafutwa kwenye daftari la Msajili wa Makampuni baada ya miezi miwili kuanzia tarehe **30 Juni, 2019** na zitakuwa zimehamishiwa kwa Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's).
3. Hivyobasi, Kuanzia tarehe ya tangazo hili, **MSAJILI WA MAKAMPUNI** hatasajili kampuni yoyote ambayo inafanya shughuli kwa lengo la kutogawana faida na ambayo haina malengo ya kukuza biashara" Promotion of Commerce".

4. Vilevile kuanzia **Tarehe 1 Septemba, 2019**, **MSAJILI WA MAKAMPUNI** hatatunza kumbukumbu za kampuni yoyote iliyosajiliwa kwa lengo la kutogawana faida na ambayo **haina** malengo ya kukuza biashara” promotion of commerce”.
5. Kwa taarifa hii tunawaomba wateja wote wawasiliane na Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ( NGO’s) kwa ajili ya kupewa utaratibu wa kuwasilisha maombi yao ya usajili kwa Makampuni ambayo yamesajiliwa na Msajili wa Makampuni (BRELA) na yanatakiwa kuhamia kwa Msajili Mashirika yasiyo ya Kiserikali ( NGO’s)kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) ya mwaka 2019.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano.**

**Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA),**

**Dar es Salaam**

**12 Julai, 2019**